**MKATABA WA PANGO**
**WA ENEO LA PLOT NO.268,270 NA 272 BLOCK B MBUGANI CHUNYA**
**NA PLOT. NO 16&18 BLOCK. C KIBAONI AREA CHUNYA**

**MKATABA HUU** umefanyika hapa **Chunya-Mbeya** leo hii tarehe 04 mwezi wa 11, 2024

**JONATHAN ESTOMIH MUNIS** wa S.L.P 37 Chunya-Mbeya ambaye kwa upande mmoja itajulikana kama "MMIRIKI" kwa upande mmoja;

**NA**

**INDIAN MINING LIMITED** wa S.L.P 37-Chunya-Mbeya ambaye atajulikana kama **(MPANGAJI)** kwa upande mwingine;

**KWA KUWA** mmiliki anamiliki maeneo yaliyopo kwenye Plot No.268,270 na 272 Block.B Mbugani Chunya- Mbeya na Plot No. 18 na 16&18 Block. C Kibaoni Chunya-Mbeya.

**KWA KUWA** mpangaji anayo nia ya kupanga nyumba maeneo yote tajwa hapo juu kwa madhumuni ya kufanya biashara ya uchakataji,uchenjuaji na uongezaji thamani madini ya dhahabu.

**KWA KUWA** mmiliki amekubali kumpangisha mpangaji maeneo tajwa hapo juu kwa kipindi cha miaka Ishirini 20 kinachoanzia tarehe 1 Mwezi December, 2023.

**HIVYO BASI, MKATABA huu unashuhudia na kudhibitisha kama ifuatavyo;**

Mpangaji na mmiriki wameridhia kuwa kodi ya pango ni shilingi za laki mbili kwa mwezi ambayo italipwa kwa kipindi cha miaka mitano mitano. Hivyo mpangaji atalipa kiasi chote siku ya kusaini mkataba huu.

I. Kwamba, mkataba huu ni kwa muda wa miezi mitatu tu na mpangaji atatumia maeneo tajwa kwaajili ya matumizi yaliyo ainishwa katika mkataba huu na si vinginevyo.

II. Kwamba, Mpangaji atalipa kiasi cha kodi ya nyumba shilingi laki mbili (TZS.200,000/=) kwa mwezi na kodi italipwa kwa kipindi cha miaka mitano kama yalivyo makubaliano kwenye mkataba huu.

III. Kwamba malipo yote yatafanyika kupitia akaunti ya mwenye nyumba baada ya kugfanaya mawasiliano na mpangaji.

IV. Kwamba, Mpangaji atayaweka mazingira ya eneo husika katika hali ya Usafi ikiwa ni ndani ya nyumba na nje, na bila kusababisha uharibifu utakaotokana na uzembe.

V. Kwamba, mpangaji atapaswa kulipa kodi zote stahiki na bili za umeme na maji kipindi chote cha mkataba huu.

**A. MASHARTI NA WAJIBU WA MPANGAJI**

i. Mpangaji anatakiwa azingatie kulipa kodi kama inavyotakiwa na kuilipa kwa wakati kama ilivyokubaliwa katika mkataba huu bila kupitisha hata siku moja;

Scanned with CamScanner

ii. Mpangaji anatakiwa azingatie usafi wa maeneo tajwa pamoja na mazingira yake na anatakiwa atumie meneo tajwa kwa shughuli amabazo zinaruhusiwa kwa mujibu wa sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

iii. Mpangaji hataruhisiwa kukodisha maeneo tajwa hapo juu kwa mtu mwingine bila ridhaa ya mmiriki wa maeneo hayo.

iv. Mpangaji kutokutumia sehemu ya maeneo tajwa kufanya biashara haramu au zinazokiuka maadili;

## B. MASHARTI NA WAJIBU WA MMIRIKI

i. Kwamba mwenye mmiriki atatakiwa kutoleta usumbufu kwa mpangaji ila kuhakikisha Mpangaji anatumia vizuri maeneo yote yalitajwa hapo juu;

ii. Mmiriki ataruhusiwa na mpangaji, kwa wakati muafaka kuingia katika kwenye maeneo pale inapobidi ili kukagua maeneo tajwa.

## C. MASHARTI YA JUMLA

Hivyo pande zote mbili zinakubaliana kama ifuatavyo:

i. Kwamba Mpangaji akitaka kuongeza muda wa kukaa kwenye maeneo tajwa atatakiwa kutoa taarifa ndani ya siku tisini (90) kwa mmiliki kabla ya mkataba wa awali kufikia ukomo;

ii. Kama pande zote mbili zitaweza kutimiza masharti ya mkataba huu kama yalivyoanishwa, hivyo mwenye mmiriki atakuwa na haki ya kumuongezea muda wa kipindi kingine cha mkataba kadiri watakavyokubaliana.

iii. Upande wowote utakaovunja mkataba huu au kukiuka masharti haya ya mkataba kabla ya kipindi cha miezi mitatu kuisha cha mkataba basi utakaokuwa umedhurika utatakiwa kulipwa gharama.

## D. USULUHISHI WA MIGOGORO:-

Iwapo kutatokea mgogoro au migogoro katika mkataba huu au sehemu ya mkataba huu, pande zote za mkataba huu zitatumia njia zozote ziwezekanazo kutatua migogoro au mgogoro huo. Endapo pande zote mbili za mkataba huu zitashindwa kutatua mgogoro au migogoro hiyo basi upande utakaokuwa umedhurika utakuwa na haki ya kupeleka mgogoro huo kwenye mamlaka yenye kuleta suluhu na kufanya maamuzi kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya muungano wa Tanzania.

**MKATABA HUU** umefanyika leo hii tarehe 04 mwezi 11, **2024** na kwa kuthibitisha hayo hapo juu, pande zote mbili zimeridhika zimekubaliana kuweka saini zao zikiwa na akili timamu bila kushurutishwa/kushawishiwa/kulazimishwa na mtu yeyote yule Mbele ya Wakili.

Scanned with CamScanner

Mkataba huu umesainiwa na **JONATHAN ESTOMIH MUNIS** leo tarehe 04 mwez 11 2024. } ________ MMIRIKI

**Mbele yangu;**
Jina Kamili: ANSIBERT RUGAIBURA
Sahihi: ________
Anuani: DAR ES SALAAM
Cheo : WAKILI

Ansibert Rugaibura Jovin
Box 65107 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Mkataba huu umesainiwa na
**INDIAN MINING LIMITED**
leo tarehe 04 mwezi 11, 2024 } MPANGAJI

INDIAN MINING LIMITED
P.O. Box 37
CHUNYA
MBEYA - TANZANIA

Jina Kamili: RASHPAL SINGH
Sahihi: ________
Anuani: 37-CHUNYA
Cheo : MKURUGENZI

**Mbele yangu;**
Jina Kamili: ANSIBERT RUGAIBURA
Sahihi: ________
Anuani: DAR ES SALAAM
Cheo : WAKILI.

Ansibert Rugaibura Jovin
Box 65107 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Scanned with CamScanner